

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**UNAMA ni Chombo cha Kisasa na Wakala wa Ujasusi wa Dola za Magharibi; Kazi yake nchini
Afghanistan Lazima Ikomeshwe Mara Moja!
(Imetafsiriwa)**

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kauli moja liliidhinisha azimio la kuongeza muda wa Misheni ya Usaidizi ya Umoja wa Mataifa nchini Afghanistan (UNAMA) kwa mwaka mwingine. Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa alitaja kuregeshwa kwa uwepo wa UNAMA nchini Afghanistan kuwa ni "muhimu" na kusema kwamba jumuiya ya kimataifa inataka "kuzidisha maingiliano na kujenga imani" na Taliban.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Afghanistan inalaani kuongezwa kwa muda wa UNAMA na inaichukulia kuwa misheni ovu na chafu - ambayo mwendelezo wake ni hatari kwa watu wa Afghanistan unaolenga kuwapurukusha watawala wa sasa kutokana na utabikishaji kamili wa Uislamu.

Kazi ya UNAMA kwa hakika inahusishwa na uvamizi na sera za dola kuu nchini Afghanistan. Wakati nchi hiyo ilipokuwa chini ya udhibiti wa Marekani, kazi ya UNAMA iliidhinishwa na Baraza la Usalama mwaka 2002 kwa lengo la kuleta mageuzi ya kisasa, kiuchumi na 'yenye msingi wa thamani' nchini Afghanistan. Kwa hakika, UNAMA imekuwa tawi la kisasa na kithaqafa la ukoloni katika kipindi cha miaka 20 iliyopita ya Jamhuri ambayo imefanya juhud kubwa kuongoza ajenda za usekula na mageuzi ya kisasa kwa msingi wa demokrasia huku ikidhoofisha maadili ya Kiislamu nchini. Baada ya kuondoka kwa aibu kwa vikosi nya Marekani na NATO, mashirika ya kisasa na kitamaduni na misheni ya uvamizi huo pia yalipaswa kuondolewa kutoka kwa uso wa Afghanistan. Lakini sio tu kwamba misheni hii hatari iliendelea, leo UNAMA inafanya kazi kama mwavuli mkubwa unaojumuisha mashirika 20, fedha na programu zinazolenga kukuza maadili ya kiliberali na mageuzi ya kisasa ya kidemokrasia chini ya pazia la misaada ya kibinadamu.

Kilichotuletea majuto na wasiwasni zaidi ni kwamba msemaji rasmi wa serikali ya Afghanistan amekaribisha kuongezwa muda kwa mamlaka ya UNAMA. Alisema katika Televisheni ya Taifa ya Afghanistan inayomilikiwa na Serikali: "InShaAllah (Mungu akipenda), itakuwa kwa manufaa ya Afghanistan kwa sababu Afghanistan inahitaji kuwasiliana na nchi na mashirika. Katika suala hili, UNAMA inaweza kuwa kama kichocheo cha kuimarishta uhusiano." Kwa hakika Umoja wa Mataifa, misheni na mashirika yake ni mashirika ya kijasusi na vyombo vya kisasa vya dola za Magharibi ambayo shughuli zake hazina taathira nyingine isipokuwa uovu na masaibu. Kudumisha uhusiano wowote na kuwa na mtazamo chanya kwa Umoja wa Mataifa na taasisi nyingine za kimataifa ni kosa kubwa la kisasa lenye matokeo hatari.

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَخَذُوا بَطَانَةً مِنْ دُونِكُمْ لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُؤُوا مَا عَنِتُّمْ قَدْ بَدَتِ الْبَعْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَآ لَكُمُ الْأَيَّاتَ
إِنْ كُلُّنَا نَعْلَمُ]

"Enyi mlio amini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasio kuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayo kudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni Ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini." [Aali-Imran: 118]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
Wilayah Afghanistan**